

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)



## MKATABA WA KAZI YA UFUNDI WA KUTENGENEZA NA KUFITISHA MADIRISHA NA MILANGO YA GRILL UJENZI WA CHUO CHA VETA MKINGA

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 09 mwezi 03 2022

### KATI YA

Mkurugenzi wa Kanda, VETA Kanda ya Kaskazini, S.L.P. 1738, Moshi, ambaye anaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802, Dodoma (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

### NA

Florian Peter Mboya wa Muheza-TANGA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri anajenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya michoro pamoja na mchanganuo wa kazi za Ujenzi vinavyoonyesha kazi zitakazofanyika.

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO;

### 1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, gharama za ufundi ni Shilingi za Tanzania 16,333,000.00 (Milioni Kumi na Sita laki tatu thelathini na tatu elfu tu.)

Fundu atafanya kazi ya kutengeneza na kufitisha madirisha na milango ya grill kwa majengo kumi na tatu (13) kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

